

SIRI YA MAFANIKIO YOYOTE

Moja ya wakufunzi wangu aliwahi kuniambia kuwa hakuna kitu cha ziada kinachowafanikisha watu zaidi ya tabia zao walizojijengea na kuzishi.

Utofauti kati ya mtu aliye fanikiwa na ambaye hajafanikiwa ni tabia zao.

Hivi unajua hata matajiri wakubwa huwa nao wanakopa? Ila matumizi ya mikopo yao yanaendeshwa na tabia zao na wanajikuta ni wanufaikaji wakubwa wa mikopo hiyo.

Wengi tunatumia vizuri kanuni za kuzalisha fedha ila hatutumii kanuni kwenye kuzitumia hizo fedha.

Wengi wetu tunatumia tabia kwenye matumizi kuliko kanuni au sheria za fedha. Na Baba yangu iliwahi kuniambia kuwa mahali pakikosekana sheria au utaratibu hapawezi kukosa vurugu.

Sasa wengine tumejisababishia vurugu kwenye matumizi ya fedha kiasi kwamba tumeingia kwenye madeni. (sina maana ya kukukashfu ila natamani ufahamu tatizo lako lilipo anzia)

Mtu mmoja aliwahi kusema mafanikio ni kitu unachokivutia kulingana na mtu uliyeamua kuwa, hivyo mafanikio hayana cha ziada zaidi ya tabia.

Ukijifunza tabia za watu waliofanikiwa na wewe takuwa mmoja wao, lakini kwenye kitabu hiki sihitaji kukupeleka mbali ila nahitaji nikusaidie namna ya kutengeneza tabia ambazo zitakusaidia kutoka kwenye maisha ya madeni.

Kuna tabia unapaswa uziue na tabia unazopaswa kuzizalisha ili zikusaidie kuchomoka kwenye minyororo ya madeni.

Nakuhakikishia ukiwajibika ipasavyo sawa na maongozo ya kitabu hiki hutachelewa kuwa huru mbali na madeni.

Karibu kwenye uhuru wako mbali na madeni, ni maombi na matumaini yangu kwamba baada ya kusoma na kuzitumia kanuni nilizokuandikia humu utakuwa huru mbali na madeni. **karibu**